BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Pili – Tarehe 28 Novemba, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Taarifa ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kwa mwaka 2023/2024.

### Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi :

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) kwa mwaka 2023/2024.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora juu ya Taarifa ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Taarifa ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi juu ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) kwa mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

96. MHESHIMWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Taasisi zetu za Umma zinapaswa kuwa na vifaa vya kujikinga na maafa ikiwemo vifaa vya kuzimia moto.

(a) Je, ni kwa kiasi gani taasisi zetu zinalitekeleza agizo hili.

(b) Je, ni hatua gani za kisheria zinapaswa kuchukuliwa kwa taasisi ambazo hadi sasa bado hazijaweka vifaa hivi ndani ya ofisi zao.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

99. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa usafi ni afya pia ni uchumi kwa nchi yetu. Na kwa kuwa maeneo mengi katika shehia zetu za Zanzibar yanakabiliwa na changamoto ya kukosa vifaa vya kisasa vya kuzoa na kusafirisha taka hizo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto hiyo kwa maslahi ya afya na uchumi wa Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

103. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi za kuyafungua maeneo huru ya kiuchumi (special economic zones) kama vile eneo huru maalum la Micheweni kwa ajili ya uwekezaji. Pamoja na juhudi kubwa za Serikali katika kulifungua eneo hilo, ipo changamoto kubwa ya eneo hilo kukosa bandari (sea port) itakayokuwa na uwezo wa kurahisisha shughuli za uwekezaji.

(a) Je, uwezo wa bandari mpya ya Shumba utaweza vipi kuimarisha shughuli za eneo hili huru la kiuchumi la Micheweni.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kufanya tathmini ya kina juu ya uwezekano wa bandari ya Shumba kuwa na uwezo wa kupokea meli kubwa za mizigo ili kusaidia eneo hilo la uwekezaji.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kuimarisha miundombinu ya usafirishaji katika eneo hilo huru la kiuchumi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

2. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Asilimia kubwa ya wananchi wameshajihishika kufanya shughuli za kifedha kwa kutumia njia ya simu.

Je, Serikali imefanya tathmini ili kujua ni kwa kiasi gani miamala ya fedha kwa njia ya simu (mobile transactions) inachangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

44. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya kazi kubwa ya kuleta mageuzi katika sekta ya miundombinu bora na ya kisasa.

(a) Je, Wizara yako inajiandaa vipi kutoka katika ufaulu wa matokeo (grade) kuelekea kwenye ufaulu wa uchumi na ajira.

(b) Ni zipi faida na hasara za kumpima mwanafunzi kwa mfumo wa grade.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

31. MHESHIMWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Mikakati gani mpaka sasa inatumika kulifanya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kupunguza utegemezi kutoka Serikalini.

32. MHESHIMWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Tathmini iko vipi juu ya mauzo na faida inayopatikana kutokana na mauzo ya magazeti ya Serikali likiwemo miongoni mwao gazeti mahiri la Zanzibar Leo.

(b) Ni kwa asilimia ngapi Serikali imeweza kupunguza changamoto zinazolikabili gazeti la Zanzibar Leo kwa sasa kiasi ya kutoleta ufanisi kiutendaji.

(c) Je, upo vipi uhifadhi wa magazeti ya Serikali, ikiwa ni pamoja na gazeti la Zanzibar Leo, kwa kipindi cha takribani miaka 20 iliyopita.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

78. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na mkakati mzuri wa kufanya utambuzi na usajili wa ardhi katika maeneo yaliyopangwa.

(a) Je, katika kuitambua na kuisajili ardhi ya Zanzibar, ni maeneo mangapi yaliyopangwa yameshatambuliwa.

(b) Je, hali ya usajili wa ardhi ya Zanzibar iko vipi kwa sasa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

65. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kiasi gani biashara ya chuma chakavu inaathiri miundombinu katika baadhi ya miradi inayotekelezwa.

66. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Magari yenye uzito kuanzia tani 10 yanayobeba mchanga, mawe na kifusi yamekuwa yakisababisha ajali nyingi hususani kwa gari ndogo ndogo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti kadhia hii.

**Wizara ya Afya:**

21. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Kwa ujumla wake kwa sasa nchi yetu ina madaktari wangapi wa kiume na wangapi wa kike kwa mujibu wa takwimu za Serikali.

(b) Je, tofauti hiyo ni ya kimkakati au ni ya kimatokeo tu.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

85. MHESHIMIWA CHUM KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali inapiga vita matumizi mabaya ya rasilimali zisizorejesheka.

Je, ni changamoto zipi kubwa zinazoikabili Wizara yako katika kulinda rasilimali zisizorejesheka.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

13. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Je, Wizara yako inamiliki matrekta mangapi ambayo yanatumika kuwahudumia wakulima wadogo wadogo katika shughuli zao.

(b) Tathmini iko vipi juu ya idadi ya matrekta na mahitaji ya huduma hiyo kwa wakulima wadogo wadogo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

125. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Jumuiya ya Nchi zilizo kwenye Mwambao wa Bahari ya Hindi (Indian Ocean Rim Association – IORA) ni moja ya jumuiya muhimu kwa mustakabali wa kuimarisha sera ya uchumi wa buluu Zanzibar, ikilenga kuimarisha uvuvi, usafirishaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia.

(a) Je, ni kwa namna gani Serikali imefaidika na Jumuiya ya nchi zilizo kwenye Mwambao wa Bahari ya Hindi.

(b) Je, ni kwa namna gani miongozo ya IORA kuhusu masuala ya ulinzi na usalama wa bahari kuu imeisaidia Zanzibar.

(c) Ni upi mkakati wa Serikali kupitia miongozo ya IORA na mikataba mingine ya kikanda na kimataifa katika kupambana na uhalifu wa uvuvi haramu.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

56. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Ni nani Banja Faraja katika historia ya Zanzibar.

(b) Kaburi la mtu huyu linapatikana wapi.

(c) Kipi kilichopelekea bwana huyu kuwa ni miongoni mwa watu wanaoigusa historia ya nchi yetu mpaka kufikia historia yake kuandikwa na kurithishwa kizazi na kizazi.

## IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Taarifa ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi :**

Taarifa ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) kwa mwaka 2023/2024.

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**

**Zanzibar,**
**27 Novemba, 2024.**